GLOBAL AFRICA

# Wito wa Makala, Toleo la 4

## Makisio ya Sasa na Siku zijazo: Afrika, Uundaji wa Maarifa na Changamoto za Ulimwengu

**Wahariri**:
Uchenna Okeja, Chuo Kikuu cha Rhodes: u.okeja@ru.ac.za
Faisal Garba, Chuo Kikuu cha Cape Town: faisal.garbamuhammed@uct.ac.za

Masomo ya Afrika ni miongoni mwa mambo mengine, mbinu ya uchunguzi inayojaribu kufikiria kuhusu Afrika na ulimwengu kwa ujumla, mipaka ya teleolojia ya kisasa inayodhania Afrika na Waafrika kama nafasi na nyanja za unyama au kabla ya ujio wa ubinadamu, ambazo zinahitaji bora zaidi, kusafishwa, kuletwa kwa kasi na kujumuishwa katika safari ndefu ya historia ikiwa haijafutwa kabisa, kutishwa na kutupwa. Kwa sababu hii, ni kweli kueleza kuwa kukataliwa kwa umiliki wa mamlaka ya kikoloni juu ya uwepo, kufikiri, matarajio ya sasa na fikra ya siku zijazo ni sharti awali la kujihusisha na ulimwengu kwa mkabala wa masomo ya Kiafrika. Kwa kifupi, kilicho hatarini katika taaluma hii ni ufahamu wa hitaji la msimamo wa maarifa unaosisitiza "kujitenga" kutoka kwa mifumo ya kidhana iliyoenea, iliyojengwa katika misingi ya kudhoofisha utu na unyonyaji wa wengine- hasa wasio weupe na wasio binadamu. Licha ya huu msimamo wa kimaarifa, hata hivyo, hali ambazo tunapaswa kushiriki au kutoshiriki na Magharibi ya kisasa inayoonekana kuenea imesalia kuwa eneo la kutokubaliana kati ya mila ya wasomi wa Kiafrika. Wakati mila za baada ya ukoloni, *Afropolitan* na *Afrofuturist* kwa mfano, zinazingatia uwezekano wa usasa tofauti usiopinga Uafrika na Usasa, mikabala mingine, yaani mila za *Afrocentrist, Endogenist* na uhuru zinataka uwezekano wa kujitenga na usasa/ukoloni ambao wanadai unapatikana tu Afrika, unasalia kuwa kitendawili. Ambacho bado hakijashughulikiwa hivyo basi, ni jinsi tunavyoweka katika mazungumzo, mijadala ya mila hizi tunapofikiria Afrika kama eneo la nadharia ya kimataifa iwapo tunachukua uhusiano wa kihistoria ya bara hili na miungano inayoendelea katika michakato ya kimataifa.

Haya yanazua angalau maswali matatu:

1) Je, ni mawazo na dhana gani tunaweza kukuza/kuendeleza kutoka nafasi za Kiafrika ili kushughulikia (Afrika nzima na kiutekelezaji) changamoto za kimataifa za kijamii, kisiasa na kimazingira?
2) Je, tunaweza kufikiria vipi matatizo ya kimataifa, hasa ya *Anthropocene* iwapo tutayafikiria kutoka ndani ya Afrika?
3) Je, matokeo ni yapi kwa Afrika, iwapo itakuwa chanzo cha suluhisho ya changamoto za ulimwengu mzima kinadharia na vitendo?

Haya maswali matatu yanaonyesha umuhimu wa kuifanya Afrika kuwa kitovu cha nadharia ya kimataifa. Ili kufikia lengo hili, tunahitaji kufikiria jinsi ya kurekebisha mwelekeo wetu kwa kufikiri kwa makini. Hili litajumuisha kuainisha njia mpya za kutathmini upeo wa bidii ya kinadharia katika taaluma tofauti ili kwa mfano, tuweze kufahamu kikamilifu mwelekeo wa kimataifa wa nadharia iliyokuzwa katika anga za Afrika ambayo inachangia katika utatuzi wa changamoto Afrika na ambazo zina athari kimataifa. Hatua ya kuanza ya kufikiria kimataifa kutoka Afrika inalenga umakini kwa kile kinachoitwa 'maswali ya jinsi gani'- yaani, maswali kuhusu jinsi ya kufikiria na wala sio tu kile tunachofikiria. Katika kutafuta mwelekeo mpya wa kufikiria ili kutuwezesha kuifanya Afrika, kituo kilichochukuliwa kwa mzaha, kuwa cha uzalishaji wa nadharia za kimataifa, tunaafikia malengo mawili- tunatunga suluhisho kwa matatizo ya sasa katika ulimwengu wa Afrika na tunaonyesha njia mpya ya kuelewa matatizo ya kimataifa kama matatizo ya pamoja ya binadamu ambayo yanaweza kutatuliwa kwa kutumia rasilimali kutoka kila sehemu ya dunia.

Mojawapo ya changamoto kuu katika kuafikia na malengo haya ni mbinu. Changamoto ya mbinu haiwezi kuchukuliwa kimzaha kwa sababu lazima tuwe na uhakika wa mwafaka wa vifaa tunavyotumia katika fikra zetu iwapo tunatarajia kubadili au kuweka wazi umuhimu kimataifa dhana ambazo zinapatikana katika anga za Kiafrika. Lazima pia tuhakikishe kuwa dhana kuu ni mwafaka ili kutuwezesha kujenga mwelekeo mpya wa kufiria ambao tunatamani.

Kwa misingi ya usuli huu, toleo hili la Jarida la *Global Africa* inachunguza swala la uundaji wa maarifa katika ulimwengu wa Afrika. Toleo hili linanuia kuchangia katika ufufuaji wa usomi wa sayansi ya jamii na ubinadamu huku tukijumuisha sayansi ya mazingira katika mazungumzo yao, ili kuunda uelewa mpya wa Afrika na Dunia nzima. Linakaribisha michango inayoshughulikia changamoto zinazokabili ulimwengu kwa sasa, kama vile maana na athari za kipindi cha kidijitali, swala la uhamaji na changamoto za umasikini, tishio la kila wakati kwa ukosefu wa usalama duniani- kutoka kwa vitisho kwa uwepo wa binadamu hadi shughuli za uharibifu za vikundi vyenye silaha. Tunakaribisha waandishi kuwasilisha michango inayohusiana na masuala ya dharura zaidi duniani, mahususi, uhusiano uliopo baina

ya sayari na jamii yetu (swala ambalo haliwezi kamwe kutenganishwa na michakato ya ukoloni na ufikiaji rasilimali) pamoja na nadharia za maarifa zinazozingatia Afrika na zinazoruhusu njia mbadala ya kufikiria uhusiano wetu na dunia.

Pia tunakaribisha michango inayohusu majibu ya Afrika kwa changamoto zifuatazo na nyingine nyingi:

- Mawazo mapya ya mradi wa kufikiria ili kukabiliana na ulimwengu ulio katika hali ya mabadiliko
- Mifumo ya taasisi na mashirika yanayohitajika kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni ulimwenguni
- Maarifa yatakayotuwezesha kupendekeza suluhisho muhimu na mwafaka kwa mabadiliko katika mabadiliko ya tabia-nchi, kawi na umasikini wa kawi ulimwenguni kwa njia ya kweli
- Njia mpya za kurekebisha dhana za zamani kama vile uafrika, uondoaji ukoloni, ukombozi, uhuru n.k.
- Uvumbuzi wa akili bandia na athari zake katika mitindo ya maisha
- Vijana wa Kiafrika kama washiriki wa kimataifa
- Mabadiliko katika ruwaza za upinzani na ukiukwaji wa haki za binadamu kutoka pembeni
- Njia za kufunza na kufunzwa na changamoto za kipindi cha sasa cha historia
- Njia mpya za uamuzi katika sera za umma

Ikisiri unaopendekezwa unapaswa kuwasilishwa moja kwa moja kwa wahariri wa toleo maalum kwa uzingativu awaliredaction@globalafricapress.org

Ratiba tarajiwa:

• Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Ikisiri  (maneno 500): **Machi 15, 2023**

• Kufahamishwa kuhusu kukubalika kwa Ikisiri : **Machi 23, 2023**

• Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha makala: **Juni 10, 2023**

• Uchapishaji wa Toleo: **Disemba 16, 2023.**

Kwa maswali kuhusu toleo maalum, tafadhali wasiliana na wahariri:
redaction@globalafricapress.org